NAMBA (2)

تَحْرِيْمُ

اللَّطْمِ وَالنِّيَاحَةِ وَلُبْسِ السَّوَادِ عَلَى الْمُصِيبَةِ

مِنْ كُتُبِ الشِّيْعَةِ الْإِثْنَيْ عَشَرِيَّةِ

UHARAMU

WA KUJIPIGA MAKOFI, KUNYANYUA SAUTI (ZA KUOMBOLEZA) NA KUVAA NGUO NYEUSI KWA KUPATWA NA MSIBA

(KUTOKA KWENYE VITABU VYA MASHIA)

Ameikusanya:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

1. Imepokewa kwamba Ally -Allaah amridhie- amesema wakati alipowausia wafuasi wake:

"لَا تَلْبِسُوا السَّوَادَ فَإِنَّهُ لِبَاسُ فِرْعَوْنَ"

"Msivae mavazi nyeusi, kwa sababu ni mavazi ya Firauni"[1].

Na aliulizwa Imam As Sadiq kuhusu mtu kuswali na kofia nyeusi akasema:

"لَا تُصَلِّ فِيهَا فَإِنَّهَا لِبَاسُ أَهْلِ النَّارِ"

"Usiswali nayo kwa sababu hilo ni vazi la watu wa motoni"[2].

2. Amesema Abu Ja'far Muhammad Bin Hasan At Tuusi (460h)

"البُكَاءُ لَيْسَ بِهِ بَأْسٌ، وَأَمَّا اللَّطْمُ وَالْخَدْشُ وَجَزُّ الشَّعْرِ وَالنَّوْحُ فَإِنَّهُ كُلُّهُ بَاطِلٌ مُحَرَّمٌ إِجْمَاعًا"

"Hapana vibaya kulia (kwa sababu kufiwa), ama kujipiga makofi, kujikwaruza kwa makucha, kukata nywele na kunynayua sauti kwa kuomboleza, hakika yote hayo ni batili, ni haramu kwa maafikiano ya maulamaa wote (wa Shia)"[3].

3. Na Al Majlis ameitaja inayosema:

"وَإِنَّ النَّائِحَةَ إِذَا لَمْ تَتُبْ قَبْلَ مَوْتِهَا تَقُوْمُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَعَلَيْهَا سِرْبَالٌ مِنْ قَطِرَانٍ، وَدِرْعٌ مِنْ جَرَبٍ"

"Mwanamke mwenye kuomboleza asipotubia kabla ya kufa kwake, atasimama siku ya kiama hali ya kuwa juu yake kuna nguo ya lami, na kanzu ya ukurutu"[4].[5].

Miongoni mwa vituko vyao kuhusu mavazi ya rangi nyeusi wanasema: **"Kuvaa viatu vyeusi husababisha mambo matatu: kunadhoofisha macho, kurefusha dhakari na kudumisha huzuni"[6].**

---

[1]- Kitabu: [Wasaailu Sshii'a] cha Muhammad Bin Hassan Al Hurrul 'Aamiliy (Jz. 1, Uk. 111) na [Man Laa Yahdhuruhul Faqih] cha Muhammad Bin Ally Bin Hussein Ibn Baabawaihi Al Qummi (Jz. 1, Uk. 2).
[2]- Kitabu: [Man Laa Yahdhuruhul Faqih] (Jz. 5, Uk. 42) na [Wasaailu Sshii'a] (Jz. 3, Uk. 111)
[3]- Kitabu: [Al Mabsuut] (Jz. 1, Uk. 231).
[4]- Kitabu: [Bihaaru al Anwaar] (Jz. 22, Uk. 451)
[5]- Asili yake ni hadithi sahihi ipo kwenye sahihi Muslim (934.)
[6]- Kitabu: [Usuulul Kaafi] (Jz. 6, Uk. 465).

JE, NI KWA AJILI YA KUMTETEA HUSSEIN AU KUNA MALENGO MENGINE?:

Ndugu msomaji, ukweli ni kwamba Nchi ya Iran inatoa msada mkubwa kuhakikisha kwamba maombolezo haya yanafanyika sehemu kiubwa duniani, kwa madai ya kumbukumbu ya kifo cha Hussein Bin Ally Bin Abi Twalib-Allaah amridhie Yeye na Baba yake-,Hussein aliuwawa kwa dhulma na wafuasi wake wa Mji wa Kufa, baada ya kumuandikia barua takriban Elfu ishirini wakimuita kwenda katika mji huo wa Kufa huko nchini Iraq.

Hapa nitataja maneno ya Khomein sheikh wao mkubwa na kiongozi wao wa mapinduzi ya Iran akielezea malengo ya kumbukumbu za 'Aashuraa:

"إِنَّ الْبُكَاءَ عَلَى الشَّهِيْدِ يُعدُّ إِبْقَاءً عَلَى اتِّقَادِ جَذْوَةِ الثَّوْرَةِ وَتَأَجُّجِهَا"

"Hakika kumlilia shahidi (Hussein) huzingatiwa ni kuwasha moto wa mapinduzi (ya Iran) na kuchochea". Kitabu: [Nahdhwat 'Aashuraa] (Uk. 3).

Kadhalika amesema tena:

"يَنْبَغِيْ لَنَا إِحْيَاءَ مُحَرَّمٍ وَصَفَرٍ بِذِكْرِ مَصَائِبِ أَهْلِ الْبَيْتِ (عَلَيْهِمُ السَّلاَمُ)؛ فَبِذِكْرِ مَصَائِبِهِمْ بَقِيَ هَذَا الدِّيْنُ حَيًّا حَتَّى الآنَ".

"Tunapaswa kuhuisha kumbukumbu za Muharram na Safar, kwa kutaja majanga yaliyowasibu Ahlul Bayt -Alayhimus salaam-, na kwa sababu ya kukumbuka majanga kumeifanya dini hii ya (Ushia) ibaki hai mpaka sasa"[7].

Hitimisho: Malengo ya maombolezo haya, kwanza ni kuimarisha mapinduzi ya Iran na kutia chuki zaidi kwenye nyoyo Mashia kuzidi kuwachukia Sunni, kwa sababu asili ya nchi ya Iran ni Masuni wa madhehebu ya Imam Shafi' -Allaah amrehemu- Khomein na washirika wake wakawauwa na kuchukua nchi kimabavu na baadae kuasisi Dola ya Kishia, na mpaka leo mji mkuu pekee mbao hakuna msikiti wa Sunni ni Tehran tu.

Arafat Bin Mahmoud
Jumatano 11/Muharram/1446h

[7]- Kitabu: [Nahdhwat 'Aashuraa] (Uk. 76).